



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya)



Email- ded.itigidc@singida.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Itigi
01 Barabara ya Halmashauri
S.L.P 70,
43483 ITIGI - SINGIDA.

Unapojibu tafadhali taja
Kumb.Na. HW/ITG/S1/22 VOL IV/39.

27 Disemba, 2023.

Kwa Wananchi wote.

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Itigi inapenda kuwatangazia waombaji kazi ya **Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja II nafasi 3** zilizotangazwa tarehe **27 Novemba 2023** katika tangazo lenye **Kumb. Na.S1/22 VOL IV 27**, kuwa usaili umepangwa kuanyika kama ifuatavyo:

a) Mwandishi Mwendesha Ofisi Daraja II Usaili wa vitendo utafanyika tarehe **04 Januari 2024** na usaili wa mahojiano ya ana kwa ana utafanyika tarehe **05 Januari 2024** katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

2. Aidha, wasailiwa wote walioitwa katika usaili wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:

i. Wafike na vyeti halisi (Original Certificate) pamoja na nakala ya vyeti husika siku ya usaili kama Cheti cha kidato cha nne, cheti cha Taaluma, Cheti cha kuzaliwa, Kitambulisho cha Taifa (NIDA), Kitambulisho cha mkazi, hati ya kusafiria, kitambulisho cha mpiga kura au barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kata/Mtaa/Kijiji iliyo na picha ya mhusika na iwe imegongwa muhuri.

ii. Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itigi haitahusika na gharama za chakula, malazi na usafiri kwa waombaji wote walioitwa kwenye usaili.

iii. Ofisi hii haitawasiliana na wasailiwa kwa njia ya **SIMU**, hivyo wasailiwa wanatahadharishwa na utapeli unaweza kutokea kwa kupigiwa simu na matapeli na kupewa maelezo mengine.

iv. Waombaji ambao majina yao hayaonekani katika Tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo wajaribu kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa kwa kuzingatia vigezo, pamoja na tangazo hili orodha ya waombaji wenye sifa walioitwa kwenye usaili imeambatishwa.

v. Wasailiwa wote mnaombwa kuzingatia muda uliopangwa.

3. Tangazo hili limetolewa na



John K. Mgalula

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI

Nakala: Katibu

Ofisi ya Rais

Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma

S.L.P 2320

Dodoma.

-Mbao zote za matangazo

HALMASHAURI YA WILAYA YA ITIGI**ORODHA YA MAJINA YA WALIOITWA KWENYE USAHILI**

NA	JINA KAMILI	SANDUKU LA POSTA
1	SHIJA REUBEN SIMBILA	P. O BOX 1 IGUNGA
2	SUZAN BARIKI KOMBE	P. O BOX - 2890 DODOMA
3	RESTITUTA ALLOYCE MARMO	P. O BOX - 1534 SINGIDA
4	REGINA MATHIAS MATHAYO	P. O BOX - 505 MTWARA
5	MILEMBE ENOS JOHNSON	P. O BOX - 73 CHATO GEITA
6	ADELAIDA JOSEPHAT MCHILO	P. O BOX - 36 MOROGORO
7	JULIANA RAMADHANI JUMANNE	P. O BOX - 1696 MOROGORO
8	SOPHIA KANOLO JOHN	P. O BOX - 140 CHATO